Mchango wa Mh Benjamin William Mkapa kwenye sekta ya Utalii

Mwandishi: Zakia Hamdani Meghji

Mh Benjamin William Mkapa alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya tatu iliyodumu miaka kumi, 1995 – 2005.
Nilibahatika kuwa Waziri katika kipindi chote cha uongozi wake. Kwanza kwa mwaka mmoja kama Waziri wa Afya na baadaye kwa miaka tisa kama Waziri wa Maliasili na Utalii. Imani yake kwangu, na naamini utendaji wangu, ulipelekea kuwa Waziri aliyedumu muda mrefu kuliko mawaziri wengine wote mpaka hivi sasa katika wizara hii. Alikuwa Hodari kunielekeza, kuniongoza na kuniamini.

Si rahisi kuandika juu ya alama alizoacha Mh Mkapa na ukaridhika kufanya hivyo. Hata hivyo nitajitahidi kuweka kumbukumbu chache za aliyoyafanya na alama alizoacha katika sekta ya Maliasili na Utalii.

Mh Mkapa alifanya mengi, alikuwa kiongozi aliyeheshimiwa ndani na nje ya nchi. Alikuwa Mwanadiplomasia wa hali ya juu, mwandishi mzuri, mfuatiliaji mahiri mwenye kujali muda na kujali zaidi matokeo kuliko maneno mengi. Alitaka nyaraka za Baraza la Mawaziri ziwe fupi, michango isiwe ya kurudiwa rudiwa na kufanya maamuzi ya haraka. Pamoja na hayo akizungumza “kimombo” (kiingereza) vizuri sana kama Muingereza Msomi wa Oxford. Lugha ilisaidia sana alipokuwa anazungumza na Wahisani na Waandishi wa nje katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo, na si ajabu tulifanikiwa katika kupata miradi mingi kutoka nje kutokana na ufasaha wake.

Mh Mkapa aliwaamini sana Mawaziri katika kufanya maamuzi na alikuwa hakuingilii kama hujamuuliza. Mahusiano yake na wahisani na mashirika ya kimataifa na yale yasiyo ya kiserikali yalisaidia sana katika kuimarisha Wizara niliyokuwa naiongoza ya Maliasili na Utalii. Nitajaribu kuweka alama chache ambazo zilileta maendeleo makubwa katika sekta hii.

Miundo mbinu

Sekta ya Utalii inategemea sana miundo mbinu kwani watalii wakifika nchini husafiri kwenye barabara kufika kwenye maeneo yenye wanyama na vivutio vingine vya utalii. Hifadhi za Serengeti, Ngorongoro, Tarangire, Kilimanjaro, Mikumi na kadhalika haziwezi kufikika kwa urahisi kama miundo mbinu mibovu. Watalii wakisafiri kwenye barabara mbovu zinawaumiza migongo yao na hawatavutiwa kurudi tena au kuwa mabalozi wetu wazuri wanaporudi nyumbani kwao.

Barabara kutoka Arusha kupitia Makuyuni mpaka lango la kuingia Ngorongoro ilikuwa mbovu sana, watalii waliita “Hell Road”, yaani barabara ya motoni. Kreta ya Ngorongoro ilikuwa eneo mojawapo

lililoitangaza sana Tanzania. Tulijua kuwa kama barabara hii itajengwa tungepata watalii wengi na mapato kuongezeka.

Mh Mkapa kwa kutambua hili aliwaomba Benki ya dunia (World Bank) watupatie mkopo wa kujenga hiyo barabara lakini walikataa – wakidai kuwa kujenga hiyo barabara eti kutaharibu “ecosystem”. Hata hivyo aliwaomba Wajapani kupitia balozi wake wakati huo aliyeitwa Kaitaro Sato. Japan ilikubali kujenga barabara na ilianza kujenga mwaka 2002 na kufunguliwa rasmi na Mh Mkapa akiwa Rais 2004. Magari sasa yakawa yanateleza na watalii kuongezeka na hivyo mapato kuongezeka. Si ajabu kwa hiyo kwa jitihada hizi na nyingine nitakazozitaja watalii waliongezeka maradufu kutoka Watalii kama laki tatu na hamsini (350,000) alipoingia madarakani na kufikia laki sita (600,000) alipomaliza muda wake. Hii ilipelekea pia kuendeleza eneo la Olduvai Gorge, ambalo kihistoria linatambuliwa kuishi binadamu wa kale wa kwanza. Bila ya hii barabara eneo hili lisingefunguka na kuleta watalii, hasa wale wanaopenda masuala ya kihistoria.

Jijini Dar-Es-Salaam kulikuwa na mahoteli pembezoni mwa bahari kama vile Silver Sands, Kunduchi Beach Hotel, Bahari Beach, White Sands na kadhalika. Kutokana na mvua za El Nino za mwaka 1998, barabara za kwenda kwenye hoteli hizi ziliharibika sana. Watalii na Wananchi kwa ujumla waliona tabu kwenda kwenye maeneo haya. Mh. Mkapa aliona umuhimu kuunganisha nguvu za watu binafsi (hasa wafanyabiashara wa utalii) na Serikali katika kutatua adha hii. Baada ya kuzungumza na wawezekaji wa Tanzania akafanya maamuzi na kuamua barabara hizi zijengwe. Asilimia sitini (60) kutoka Serikalini na asilimia arobaini (40) kutoka kwa Wawekezaji. Barabara hizi pia zilifungua maeneo yaliyokuwa karibu na hoteli hizi.

Mafunzo

Watalii wakija nchini hukaa kwenye mahoteli. Hulala, hupata chakula na burudani mbalimbali. Kwa maana hii, huduma nzuri kwenye hoteli hizi ni muhimu sana. Tanzania ilikuwa haijatilia mkazo suala hili, na hivyo tulibaki kulalamika pale tulipokuta Wafanyazi wa nchi Jirani wanaajiriwa kwenye mahoteli yetu. Suala hili lilimkera sana Mh Mkapa na katika ziara zake za Ulaya alizungumza na Serikali ya Ufaransa juu ya uwezekano wa kujenga Chuo cha kisasa chenye hadhi ya kimataifa ili kutoa mafunzo kwa vijana wetu katika fani ya upishi na uhudumiaji wa watalii kwa ujumla. Kimsingi ombi hili lilikubaliwa na akanitaka niende Ufaransa mji wa Nice, ili kwa kushirikiana na balozi wa Tanzania nchini Ufaransa (wakati ule alikuwa Juma Mwapachu) tuweze kulizungumza na Wahisani kwa mapana zaidi juu ya aina ya mafunzo, chuo na msaada, na kadhalika. Tuliomba kujengewa chuo na kuwekewa vifaa vya kisasa. Matokeo yake chuo kilijengwa na ni chuo cha Taifa cha Utalii kilichopo makutano ya Samora na Shaabani Robert jijini Dar-Es-Salaam.

Uimarishaji na Ujenzi wa Mahoteli

Wakati Mh Mkapa anaingia madarakani, mahoteli mengi yalikuwa yamechakaa na mengine yamefungwa kwa muda mrefu. Hili lilipunguza idadi ya Watalii kwani kulikuwa hakuna hoteli yenye hadhi ya nyota nne au tano. Hata kule mbugani hotel zote zilikuwa kwenye hali mbaya. Kwa kupitika tume ya rais ya kurekebisha sekta ya mashirika ya umma (PSRC) mahoteli mengi yalianza kubinafsishwa. Kuna baadhi ya viongozi hawakupenda na kulaumu sana maamuzi haya, kwamba Mh Mkapa anafuata sera za kibepari. Mkapa hakusikiliza kwani alijuwa kuwa hakuna njia nyingine isipokuwa sekta binafsi kushiriki katika kukuza utalii na uchumi kwa ujumla. Kwa hivyo ubinafsishaji wa hoteli ulianza na kuendelea.

Mfano mmoja kati ya mingi ulioweka alama kubwa Tanzania na hasa Dar-Es-Salaam ni ubinafsishaji wa hoteli ya Kilimanjaro ambayo sasa hivi inajulikana kama Hyatt Kilimanjaro Hotel. Hoteli hii baada ya uhuru ndio iliyokuwa kubwa na ya kisasa. Lakini baadaye iliharibika na kufungwa kwa miaka mingi.

Serikali iliamua kuitangaza, ili apatikane mwekezaji ambaye ataijenga na kuiweka kwenye ubora ya nyota tano. Wafanyabiashara na Wawekezaji wengi waliomba wakiwemo wa ndani na nje ya nchi. Maombi yote yalichujwa. Kuna wengine waliangalia zaidi suala la uzawa kuliko uwezo wa kifedha na uzoefu katika biashara ya hoteli.

Sisi kama Wizara baada ya uchambuzi wa kina tulipendekeza apewe mfanyabiashara kutoka Dubai. Kikao cha baraza la Mawaziri katika kutoa maamuzi ya nani apewe kiligawanyika wengine wakimuunga mfanyabiashara maarufu ambaye hakuwa na uzoefu wa kuendesha hoteli. Mh Mkapa akiwa rais na Mwenyekiti wa kikao alituunga mkono. Leo hii hoteli ya Kilimanjaro ndio moja ya hoteli ya hadhi ya juu kabisa hapa nchini. Wageni wengi wa kimataifa hufikia pale mfano aliyekuwa rais wa Marekani George Bush, aliyekuwa rais wa Benki ya dunia, Prince Agakhan na wageni wengi mashuhuri. Hii ni alama kubwa ambayo Mh Mkapa ameiacha katika nyanja ya utalii.

Bologonja

Jambo lingine ambalo Mh Mkapa alituunga mkono kama Wizara ni kuhusu kutokufunguliwa kwa lango la Bologonja lililopo Serengeti. Sehemu hii iko masafa machache kusini mwa mpaka wa Kenya na Tanzania, sehemu inayopakana na Masai Mara. Lango hili limefungwa ili kulinda Watalii wanaotaka kuingia Serengeti wapitie Tanzania. Bila kufanya hivi, Watalii wengi wangefikia nchi Jirani na kuingia na kutembea tu Serengeti bila kulala au kupitia Tanzania. Hii ingeikosesha Serikali mapato.

Mh Mkapa alipata shinikizo sana kutoka Kenya na kwenye vikao vya Afrika Mashariki. Aliamua kusimama

kidete na kuunga mkono mawazo ya Wizara. Wakati wa vikao vya Afrika Mashariki alisema kuwa katika ushirikiano huu, suala la utalii liachwe na kila nchi iwe na utaratibu wake. Mpaka leo hii lango hili halijafunguliwa kutokana na sababu za kiuchumi.

Upandaji Miti

Mh Mkapa alimteua Dr Omar Ali Juma kuwa makamu wa rais na akampa kazi ya kusimamia mazingira. Kazi kubwa ilifanywa ya kupanda miti na uhamasishaji ulifanyika nchi nzima na kuliwekwa siku maalum ya upandaji miti. Suala hili limegeuka kuwa utamaduni wa Watanzania.

Wanyama pori/Uhifadhi

Mh Mkapa alikuwa anapenda sana uhifadhi. Kwa kuwa faru walikuwa wamepungua sana kutokana na ujangili, Mh Mkapa aliamua katika kipindi chake kuomba faru kutoka Afrika Kusini na kuwapandikiza ili waweze kuzaliana na kuongezeka. Faru hawa kwanza waliwekwa hifadhi ya Mkomazi na baadaye kuhamishiwa Serengeti. Matokeo yake tunayaona hivi sasa kwa faru kuongezeka. Hata baada ya kustaafu Mh Mkapa aliteuliwa katika bodi ya wadhamini ya Africa Wildlife Foundation.

Kwa kweli Mh Mkapa amefanya mengi na kuacha alama nyingi. Wapinzani watakumbuka jinsi alivyowashirikisha na hata katika kuwaalika kwenye kila hafla inayofanyika ikulu pale ambapo kuna dhifa za kitaifa.

Alitutia hamasa tukutane na Waandishi wa Habari, na alianzisha utaratibu wa kuwa na afisa Habari katika kila Wizara kama wasemaji wa Wizara. Jambo hili alilipenda sana ili kupunguza malalamiko kutoka kwa Wananchi kwa ujumla na kuwa na Serikali ya uwazi na ukweli kama kauli mbiu yake.